

Kila ninapomaliza kuoga kwa maji moto, moto.
Mwili wangu majimaji, u baridi, baridi.
Nani husababisha hilo kutendeka?
Vayu, upepo!

Maziwa ndani ya kikombe-moto sana, moto sana.
Lakini punde tu, yako tayari kwangu kuyanywa.
Nani husababisha hilo kutendeka?
Vayu, upepo!






Mapazia ya madirisha yanapapatika
na kwa upole yananipangusa uso wangu.
Nani husababisha hiki kutendeka?
Vayu, upepo!

Radi kwa umbali.

Mawingu meusi yanasonga upande wangu.

Nani husababisha hilo kutendeka?

Vayu, upepo!



Matawi yanawayawaya na majani kutetemeka.
Maua yanaanguka kwa upole.
Nani alifanya yote?
Vayu, upepo!






Mbali na nyumba, tunacheza,
lakini, naweza kunusia peremende ambazo mama anatarisha.
Nani husababisha hiki kutendeka?
Vayu, upepo!



Bilauri iliyo dirisahani,
inaanguka chini kwa kishindo.
Nashukuru Mungu sikuwa karibu.
Nani alifanya ukatili huu?
Bila shaka ilikuwa Vayu, upepo!

Firimbi inapulizwa.
Gari la moshi linaingia.
Silioni, lakini nasikia mlio wake.
Nani husababisha hilo kutendeka?
Vayu, upepo!





Haionekani. Haisikiki.
Inafanya kazi zote
bila neno.
Anaweza kuwa nani?



Bila shaka!
Ni upepo!

